TANGAZO LA SERIKALI Na. 504 la tarehe 21/7/2023

SHERIA YA MISITU,
(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 107)*

NOTISI YA MSAMAHA WA KUSAFIRISHA NJE YA NCHI MAGOGO YA MTI AINA YA MKURUNGU YA MWAKA 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Msamaha wa Kusafirisha Nje ya Nchi Magogo ya Mti Aina ya Mkurungu ya Mwaka 2023.

Msamaha wa kusafirirsha magogo

2.-(1) Kampuni ya *Paxmore Company Limited* inapewa msamaha wa kusafirisha magogo ya mti aina ya Mkurungu unaojulikana kwa jina la kisayansi la *Pterocarpus Tinctorius* kwenda nchini China pasipo kuchakatwa.

(2) Kiwango cha magogo yaliyoruhusiwa kusafirishwa nje ya nchi na Kampuni iliyotajwa katika aya ndogo ya (1) kitakuwa kama kilivyoainishwa katika aya ya 4.

Umuhimu na sababu za kutolewa kwa msamaha

3. Msamaha huu unatolewa kutokana na umuhimu na sababu zifuatazo:

(a) magogo ya Mkurungu yanayopewa msamaha wa kusafirishwa kwenda nje ya nchi bila kuchakatwa ni madogo na hivyo kusababisha ugumu wa kuyachakata hapa nchini kwa tija na kupata mbao zinazoruhusiwa kisheria kusafirishwa nje ya nchi;

(b) kukuza masoko ya magogo ya mti aina ya Mkurungu kwa kuwa masoko ya magogo haya yanapatikana nchini China na Kampuni ya *Paxmore* imeahidi upatikanaji wa masoko zaidi

ya mazao ya misitu yanayopatikana hapa nchini; na

(c) Kampuni ya *Paxmore* imeonesha kwamba upo usimamizi endelevu wa magogo ya Mkurungu na itahakikisha kwamba inatoa mchango kwa viwanda vya kuchakata mbao ndani ya nchi.

Masharti ya msamaha

4. Msamaha huu unatolewa kwa masharti yafuatayo:

(a) kiwango cha magogo ya mti wa aina iliyotajwa katika Notisi hii kitakuwa ni vipande 2,000 vyenye mita za ujazo 168.405; na

(b) aina hii ya magogo na kwa kiwango tajwa itasafirishwa kwenda nchini China.

Muda wa msamaha

5. Msamaha huu utatumika kwa kipindi cha siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii.

Dodoma,
……………, 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*